JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI

Simu : +255 (026) 2322703
Nukushi : +255 (026) 2322704
Baruapepe: km@uchukuzi.go.tz
Tovuti: https://www.uchukuzi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba, 1 Mtaa wa Ujenzi,
S. L. P 638,
40470 DODOMA

# TAARIFA KWA UMMA

## KUSOGEZWA MBELE KWA TAREHE YA MKUTANO WA KUPOKEA MAONI YA WADAU KUHUSU MAPENDEKEZO YA KUTENGENEZA KANUNI ZA USIMAMIZI WA MADHARA YA UCHOVU KWA MADEREVA ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2025

**Dodoma,**
**Tarehe 18 Desemba, 2025.**

Tunawataarifu wadau wote wa sekta ya usafiri ardhini nchini kuwa, Mkutano wa Wadau kwa ajili ya kupokea maoni kuhusu mapendekezo ya kutengeneza Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2025 uliopangwa kufanyika tarehe 22 Desemba, 2025 umesogezwa mbele hadi tarehe 8 Januari, 2026.

Mkutano huo utafanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Utalii, kilichopo Mtaa wa Shaaban Robert, Jijini Dar es Salaam kuanzia saa tatu kamili asubuhi. Tangazo hili linafuta taarifa ya mkutano wa awali iliyotolewa tarehe 9 Desemba 2025 kupitia gazeti la Mwananchi Namba 9249.

Hatua hii imefikiwa baada ya Wizara ya Uchukuzi kupokea maombi ya wadau kuwa wanahitaji muda zaidi wa kuzisoma Kanuni na kuzielewa kabla ya kushiriki kwenye mkutano.

Wizara inawakumbusha kuwa, Rasimu za Kanuni hizo zimeandaliwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na zinapatikana katika Tovuti ya LATRA **https://www.latra.go.tz/** na ofisi zote za Mamlaka Tanzania Bara.

Maoni ya maandishi yanapokelewa kupitia baruapepe **group.maoni@latra.go.tz** hadi tarehe 22 Januari 2026 ikiwa ni siku 14 baada ya mkutano.

**Wote mnakaribishwa.**

Imetolewa na:
**KATIBU MKUU – WIZARA YA UCHUKUZI**

CamScanner

Jumatano Desemba 24, 2025 Pg 6 Uhuru

# LATRA yatoa vibali zaidi mabasi mikoani

Na REHEMA MAIGALA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inaendelea kutoa vibali vya usafiri hadi kufikia 289 kwa mabasi yanayotoka Dar es Salaam kwenda mikoani ikiwa ni hatua ya kuondoa changamoto ya usafiri kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam jana, Ofisa Mfawidhi wa LATRA wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Rukia Kibwana, alisema vibali hivyo ni vya muda ambavyo mara nyingi hutolewa mwisho wa mwaka.

Rukia alisema ongezeko la abiria hao ndiyo sababu kubwa ya LATRA kutoa vibali kwa lengo la kuongeza idadi ya mabasi yaendayo mikoani.

Alisema hadi kufikia jana asubuhi tayari vibali 289 vilikuwa vimetolewa kwa mabasi yaendayo mikoa yote nchini, hatua iliyolenga kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma ya usafiri bila ya usumbufu wowote.

"Hadi leo (jana) mchana tulitoa vibali 289, unapoona watu wamejaa stendi huwa wanakuja kusubiri mabasi yao na wengine wanawahi kukata tiketi,"alisema.

Rukia alisema awali, walianza na vibali 72 lengo lilikuwa kwa mikoa mitano ambayo ilionekana ina abiria wengi zaidi ambayo ni Dodoma,Iringa,Tanga,Morogoro na Kilimanjaro.

"Hivi sasa tumetoa vibali 289 katika mikoa yote ya Tanzania na kufanya hivi tumepunguza msongamano wa abiria, wakati wa asubuhi na jioni mambo yanaenda vizuri na abiria wetu wanakwenda mikoani kama walivyopanga,"alisema.

Rukia aliwaomba wananchi kuwa na uvumilivu katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, akieleza LATRA inafahamu idadi kubwa ya watu husafiri kwenda kuungana na familia zao mikoani, hivyo mamlaka inaendelea kusimamia na kuratibu uongezaji wa mabasi zaidi kadri inavyohitajika.

"Tunaamini kipindi hiki cha kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka Krismas na Mwaka Mpya, baadhi ya wananchi wengi wanapenda kusafiri kwenda kusherehekea sikukuu hizo na familia zao,"alisema.

Hivyo alisema LATRA imekuwa ikitoa vibali vya muda kila kipindi cha msimu wa sikukuu na sherehe kubwa na kuhakikisha kuwa upatikanaji wa usafiri unakuwa wa uhakika, huku pia ikisisitiza hatua hizo zinaambatana na ukaguzi wa usalama wa magari na ufuatiliaji wa nauli zilizowekwa kisheria.

Alisema kutokana na ongezeko hilo la mabasi, msongamano wa abiria umepungua, hivyo hakuna shida ya usafiri kama ilivyokuwa awali.

**VIBALI**

Vya magari 289 katika mikoa yote ya Tanzania imepunguza msongamano wa abiria Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli.

azingatie sheria za usalama barabarani

**"Rai yangu, kila mmoja awe mlinzi wa mwingine, dereva kwa dereva na abiria kwa dereva kwa kufanya hivyo ajali zitapungua kwa kiwango kikubwa.**

# Madereva chondechonde zingatieni sheria, kanuni za usalama barabarani



Na SUPERIUS ERNEST

KATIKA kipindi hiki cha kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka, barabara huwa na wingi wa vyombo vya usafiri yakiwemo, mabasi, daladala, bajaji, bodaboda na magari ya watu binafsi.

Hali hiyo hutokana na wengi wa wananchi husafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine, kwasababu mbalimbali ikiwemo kusalimia ndugu, jamaa na marafiki.

Wengine hutumia vyombo vya usafiri kwenda sokoni kununua mahitaji mbalimbali kwa matumizi ya nyumbani katika mwelekeo wa kusherehekea sikukuu hizo.

Kwa muktadha huo, katika kipindi kama hiki barabara huwa 'bize' sana kwa idadi ya vyombo hivyo vya usafiri.

Pia, vijana hutumia magari, pikipiki na bajaji, kwenda maeneo ya starehe zikiwemo fukwe na kumbi mbalimbali kupata burudani na kufurahi pamoja.

Yote hayo ni mazuri katika kufurahi na kujipongeza katika sikukuu hizo za mwisho wa mwaka ambazo ni Krismasi na Mwaka Mpya.

Matumizi ya vyombo vya usafiri ni jambo zuri, lakini ubaya ni pale ambapo waendeshaji hukiuka sheria za barabarani kwasababu zao binafsi.

Wapo wanaoendesha vyombo vya moto wakiwa wamelewa, hatua inayochangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la ajali kipindi cha sikukuu.

Hali hiyo husababisha ajali ambazo hupoteza uhai wa watu na wengine, kupata ulemavu wa kudumu kwasababu ya uendeshaji wa vyombo hivyo uliokowa nidhamu barabarani.

Nawakumbusha kuheshimu na kutii sheria barabarani siyo ushamba, bali ni kuokoa na kulinda maisha ya dereva mwenyewe, abiria na watembea kwa miguu.

Madereva ni vyema mkaendesha vyombo vya moto kwa kufuata sheria za barabarani, maana huo ndiyo utaratibu wa uendeshaji na siyo vinginevyo.

Mkumbuke kauli mbiu yenu katika wiki hii ya maadhimisho ya usalama barabarani, isemayo, 'Familia yako inakusubiri, zingatia usalama barabarani'.

Kupuuza sheria barabarani ni kujipalia mkaa wa kifo, kwako wewe, abiria na watembea kwa miguu.

Haina faida yoyote kuendesha mwendo kasi, bila kuzingatia alama za barabarani kwani inaweza kusababisha athari kubwa vikiwemo vifo na ulemavu wa kudumu.

Waswahili walisema 'haraka haraka haina baraka' pia, mwenda pole hajikwai, ni vyema kuendesha kwa uangalifu ukafika kwa usalama hata kama ni kwa kuchelewa.

Rai yangu, kila mmoja awe mlinzi wa mwingine, dereva kwa dereva na abiria kwa dereva kwa kufanya hivyo ajali zitapungua kwa kiwango kikubwa.

Madereva wawaheshimu watembea kwa miguu na watembea kwa miguu waheshimu madereva na sheria hususan alama za barabarani zifuatwe.

Pia, madereva waheshimu na kushirikiana na mamlaka husika kudhibiti wa ajali barabarani kwa kushirikiana na trafiki na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

Pongezi kwa vyombo hivyo vya usimamizi kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya.

Naamini kwa ushirikiano wa pande hizo, ajali zitapungua, usalama utakuwepo na maisha yataendelea.

Nawakumbusha watumiaji wa vyombo vya moto, kuwa waangalifu katika kipindi hiki cha sikuuu za mwisho wa mwaka ili kupunguza ajali.

CamScanner

# Wamiliki, madereva vyombo vya moto Songwe wafundwa



*Baadhi ya washiriki wa semina elekezi kwa madereva na wamiliki wa vyombo vya moto iliyoendeshwa mwishoni mwa wiki na Mamlaka ya Uhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) mjini Songwe. (Na Mpiga Picha Wetu)*

**Na Mwandishi Wetu, Songwe**

VITENDO vya kupandisha nauli na kujaza abiria kupita kiasi kwenye mabasi vinahatarisha usalama wa abiria kutokana na ajali za mara kwa mara.

Imekuwa kawaida kwa madereva wa vyombo vya moto siku za sikukuu kuzitumia kama fursa za kujipatia kipato kwa kuvunja sheria wakipandisha nauli na kujaza abiria kupita kiasi, bila kujali kuwa wanaweza kusababisha maafa.

Mbali na hilo, pia kuna uzembe unaofanywa na baadhi ya makondakta kutowapa tiketi abiria, huku baadhi ya madereva wakifanya kazi kwa mazoea kwa kutolipia leseni zinapoisha muda.

Wamiliki wa vyombo vya moto nao wamekuwa wakikosa elimu ya matumizi sahihi ya ving'amuzi, huku wakiendelea kulalamikia madereva wao wanapobaini gari limetozwa faini za mara kwa mara.

Kutokana na makosa hayo, Mamlaka ya Uhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imeanza kutoa semina elekezi kwa madereva na wamiliki, ili kuondoa changamoto barabarani.

Mwishoni mwa wiki LATRA ilikuwa mjini hapa ikiendesha semina elekezi kwa madereva na wamiliki.

Mafunzo hayo yalishirikisha pia Jeshi la Polisi Usalama Barabaranin a Zimamoto.

Akifungua kikao hicho, Meneja wa LATRA Mkoa, Joseph Bulongo alisema lengo la mafunzo hayo ni kukumbushana na kupeana kanuni sita za sheria za uendeshaji vyombo vya moto.

Mwansheria wa LATRA Makao Makuu, Martha Ngaga alisema baada ya kuona sheria nyingi zinakiukwa, waliamua kupita kila mkoa nchini kukumbushana uwepo wa kanuni za uwezeshaji watoa huduma za usafirishaji za mwaka 2024.

Mwenyekiti wa waendesha bodaboda Songwe, Omary Mbuba, alipongeza kwa elimu waliyopewa huku akiomba ufafanuzi juu ya mawakala wa kukatisha leseni kufanya msako mitaani.

Mbuba alisema ni kawaida sasa mbia aliyepewa uwakala wa kuendesha msako mitaani na kukamata pikipiki au bajaji zisizo na leseni na kuzua taharuki na kusababisha ajali, huku mawakala hao wakivalia nguo zenye nembo za LATRA.

Elia Kibona, mmiliki wa magari licha ya kupongeza uendeshaji wa mafunzo hayo, alitaka maofisa hao kupunguza kiwango cha faini, huku akitaka wamiliki wenzake kuona umuhimu wa kufunga ving'amuzi kwenye magari yao.

Dereva Sai Padwi alihoji vigezo vinavyotumika kuwatoza faini kati ya Sh 500,000 na Sh milioni moja wanapokutwa na makosa barabarani, akisema faini hizo ni kubwa kuliko makusanyo yao.

*Kaimu* Katibu wa Chama cha Wamiliki wa *Makosta Mkoa, Elly* Songuo alisema sheria nyingi zinazotungwa *na LATRA* si shirikishi kwao, na pia mazingira ya barabara nyingi ni mabovu, hivyo kupata ukakasi wanapoambiwa watumie teknolojia zaidi.

Mmiliki wa magari ya Maribwa, Thobias Maribwa alisema magari ya kutoka Tunduma-Mbeya, abiria wengi hupandia njiani, lakini wamekuwa wakitozwa faini, kwa madai kuwa hawana *tiketi, huku akiomba ufafanuzi* wa *jambo hilo.*

*Aliongeza* pia kuwa king'amuzi kinapoharibika, dereva hana ujuzi wa kukitengeneza, akataka kujua ni njia zipi zitumike kumtambulisha dereva kuwa king'amuzi ni kibovu, ili aepuke faini.

Kuhusu faini kwa dereva anayeendesha mwendo kasi, Mkaguzi wa Usalama Barabarani wa wilaya ya Mbozi, Anthony Sabasaba alisema wamekuwa wakifanya ukaguzi mara kwa mara na kugundua makosa yanayojirudia.

Alisema dereva atakayeendesha kuanzia spidi 86 hadi 99 kisheria anatozwa faini na atakayeendesha spidi 100 na kuendelea, adhabu yake ni kunyang'anywa leseni na faini hizo zipo ili madereva waongeze umakini barabarani.

Meneja wa LATRA Mkoa, Joseph Bulongo alikanusha kuwapo faini ya Sh 500,000 na Sh milioni moja.

Alisisitiza umuhimu wa mmiliki wa chombo kufunga king'amuzi ili kufuatilia lilipo gari lake akiwa nyumbani, na hata dereva akitozwa faini atatambua kosa.

Martha alisema ni kosa mtu ama kikundi kilichopewa uwakala wa kukatisha leseni za vyombo vya moto, kufanya msako wa kukamata chombo chochote.

Alisema wakala anatakiwa kukaa ofisini kukatisha leseni na si mitaani kukamata pikipiki au bajaji na kutoza faini, akiwa na nguo zenye nembo za LATRA, akisema ni kosa kisheria.

Pia alionya madereva kutowapa vishoka au madeiwaka magari yao siku za wikiendi kwani wanaweza kusababisha ajali.

Habarileo



Desemba 24, 2025 Pg 5

# TRC yaongeza safari, mabehewa

**Na Lidya Inda**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limeongeza safari za treni na kuongeza mabehewa katika safari za reli ya kisasa (SGR), reli ya kati kwenda Mwanza na Kigoma na mikoa ya Kaskazini.

Akizungumza na HabariLEO jana, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano wa shirika hilo, Fredy Mwanjala alisema kuwa TRC imeongeza seti ya pili ya treni ya mchongoko (EMU) ambayo seti moja hubeba abiria 583, hivyo ongezeko la seti ya pili linamaanisha wanabebwa abiria 1,116 kwa wakati mmoja.

"Lakini pia katika treni yetu ambayo ina mabehewa 14 tumeongeza mabehewa mawili, sasa treni hiyo itaondoka na mabehewa 16, mabehewa hayo mawili moja linachukua abiria 48 lingine abiria 78," alieleza.

Aliongeza kuwa, "tuko tayari pia kuhudumia makundi pale tutakapoona inafaa, kwa mfano watu zaidi ya 100 au 200 wakitaka treni sisi tutaona kama inafaa kuwapa treni maalumu tutawapa treni maalumu."

Kwa upande wa treni zinazofanya safari zake kutoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya Kaskazini (Moshi na Arusha) alisema kwa kawaida treni hufanya safari zake Ijumaa na Jumatatu lakini kwa kipindi hiki cha sikukuu wameongeza treni moja ya Jumamosi ambayo itakuwa ikiondoka saa 4:00 asubuhi.

"Mikoa ya Kanda ya Kati kwa kawaida Dar es Salaam hadi Kigoma huwa tunatembeza treni ya behewa 16 lakini Serikali ya Awamu ya Sita walipatia TRC fedha kwa ajili ya kukarabati mabehewa manne na mabehewa hayo yote yamekamilika, hivyo kuelekea Krismasi na Mwaka Mpya tutatembeza behewa 20," alisema.

Alieleza kuwa lengo kubwa ni kuhudumia wananchi wanaoelekea katika eneo hilo kwa ajili ya sikukuu za mwisho wa mwaka.

MASHAMBULIZI

# Mabasi yashambuliwa njiani, polisi yakamata watuhumiwa

Na Oscar Assenga,

KOROGWE

JESHI la Polisi Mkoa wa Tanga limebaini kuwa watu waliovamia na kushambulia mabasi yaliyokuwa yakisafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Arusha, na kuvunja vioo vyake katika kipindi cha kuelekea sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, ni walevi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Muchunguzi, katika mazungumzo maalumu na Nipashe, ambapo alisema kuwa watuhumiwa wa tukio hilo tayari wameshikiliwa na Jeshi la Polisi kwa hatua zaidi za kisheria.

> **"Madereva wote wanapaswa kuzingatia sheria za usalama barabarani. Yeyote atakayebainika kuendesha kwa mwendokasi au kukiuka sheria, atachukuliwa hatua kali za kisheria bila muhali,"**

Kamanda Muchunguzi alisema tukio hilo lilitokea usiku wakati mabasi hayo yakipita katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Tanga, hali iliyosababisha hofu kwa abiria waliokuwa wakisafiri kuelekea kwenye mapumziko ya sikukuu.

"Niseme wazi kwamba walioshambulia mabasi yaliyokuwa yanatokea Dar es Salaam kwenda Arusha ni walevi. Tayari tumewakamata na tunawashikilia.

"Tunatoa onyo kali kwa wananchi wenye nia ovu kuacha kufanya vitendo hivyo, kwani tutawachukulia hatua kali za kisheria pindi tutakapowabaini," alisema Kamanda Muchunguzi.

Alibainisha kuwa Jeshi la Polisi limejipanga kikamilifu kuimarisha doria na misako katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Tanga, hususan katika kipindi hiki cha sikukuu, ili kuhakikisha usalama wa raia na mali zao unaendelea kudumishwa.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, lengo la doria hizo ni kuhakikisha wananchi wanasherehekea Krismasi na Mwaka Mpya katika mazingira ya amani na utulivu, bila vitendo vya kihalifu au vurugu zinazoweza kuhatarisha usalama.

Vilevile, alisema Jeshi la Polisi limeongeza ulinzi barabarani na kutoa wito kwa madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani, akisisitiza kuwa vitendo vya kuendesha kwa mwendokasi havitovumiliwa.

"Madereva wote wanapaswa kuzingatia sheria za usalama barabarani. Yeyote atakayebainika kuendesha kwa mwendokasi au kukiuka sheria, atachukuliwa hatua kali za kisheria bila muhali," aliongeza.




Askari wa kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Muheza mkoani Tanga jana akizungumza na abiria baada ya kutoka ndani ya basi kulikagua jana katika stendi Kuu ya mabasi wilayani humo ambapo kwa sasa mabasi mengi yanajaza abiria kutokana na sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya abiria wanakwenda mikoani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

CamScanner